**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

**MHESHIMIWA MASOUD ALI MOHAMMED**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**IMEWASILISHWA MBELE YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI,2024**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai, uzima wa afya na kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza hili leo kuwasilisha hotuba yangu ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu 12 ya bajeti ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zao wanazozichukua kudumisha amani, utulivu, mshikamano na kuleta maendeleo ya Taifa letu.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mchango wake mkubwa wa kuleta maendeleo ya Zanzibar kupitia Afisi yake hii. Katika uongozi wake Ofisi imeshatekeleza jumla ya miradi 49 ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa masoko makubwa ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini. Kwa ujumla bajeti ya kazi za maendeleo katika Afisi imefikia Shilingi bilioni 148,906,415,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikilinganishwa na Shilingi 51,307,415,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

5. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa utendaji wao mzuri wa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza azma yake ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

6. **Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa umahiri na ushupavu wako wa kuliongoza Baraza la Wawakilishi kwa hekima na busara. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma Naibu Spika kwa jinsi anavyokusaidia kutekeleza majukumu ya Baraza la Wawakilishi. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo kwa kuendesha vikao vya Baraza la Wawakilishi kwa ufanisi mkubwa.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Maryam Thani Juma Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Gando. Aidha, natoa pongezi na shukurani kwa wajumbe wa Kamati ambao ni Mheshimiwa Mussa Foum Mussa Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiwani, Mheshimiwa Abdallah Abaas Wadi Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Nungwi, Mheshimiwa Haji Shaabani Waziri Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Uzini, Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiembesamaki, Mheshimiwa Zaina Abdalla Salim Mwakilishi Viti Maalum Mkoa wa Magharibi Kichama na Mheshimiwa Panya Ali Abdalla Mwakilishi Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Unguja.

8. **Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya kazi kubwa sana ya kutushauri na kutuelekeza mambo mbali mbali yaliyolenga kuimarisha utendaji wa Serikali kwenye Afisi hii. Aidha,

Kamati imeweza kutekeleza jukumu lake la kisheria kwa kupitia mafungu 12 ya bajeti ya Afisi hii na kuchambua kwa kina mapato na matumizi pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na malengo yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa mukhtaza huo, Kamati imeridhia na imeniruhusu niwasilishe hotuba hii hapa Barazani.

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi na pongezi hizo, naomba uniruhusu sasa kuwasilisha hotuba yangu ya makadirio ya mapato na matumizi ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2024/2025 nikianzia na mapitio ya utekelezaji wa mpango, mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2023/2024.

## B. MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali

10. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lako kwa mwaka wa fedha 2023/2024 liliidhinisha kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 4,203,067,878 kutoka mafungu 12 ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali, ambapo hadi kufikia Machi 2024 jumla ya Shilingi 1,925,420,427 zimekusanywa sawa na asilimia 46 ya makadirio ya mwaka na asilimia 61 ya makadirio ya miezi tisa. **(Kiambatanisho nambari 1)**.

### Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

11. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lako pia liliidhinisha makusanyo ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya Shilingi 18,115,437,900 kwa mwaka fedha 2023/2024, ambapo hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Shilingi Bilioni 9,688,262,952 zimekusanywa sawa na asilimia 53 ya makadirio ya mwaka na asilimia 73 ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo Shilingi 4,405,717,172 sawa na asilimia 45 zilitumika kwa

kazi za maendeleo na jumla ya Shilingi 5,282,545,780 sawa na asilimia 55 zilitumika kuendeshea Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri. **(Kiambatanisho nambari 2)**.

**Upatikanaji wa fedha kwa ujumla**

12. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka fedha 2023/2024 Afisi na taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 216,243,600,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 129,893,400,000 ni mishahara, Shilingi 26,579,700,000 ni matumizi mengineyo, Shilingi 18,820,500,000 ni ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi na Wakala wa Ulinzi JKU na Shilingi 40,950,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

13. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2024, fedha zilizopatikana ni Shilingi 195,026,817,688 sawa na asilimia **90** ya makadirio ya mwaka na asilimia 120 ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo Shilingi 100,637,123,983 ni mishahara sawa na asilimia 77, Shilingi 15,470,858,554 ni matumizi mengineyo sawa na asilimia 58**,** Shilingi 12,770,139,012 ni ruzuku sawa na asilimia 68 na Shilingi 66,148,696,139 ni kazi za maendeleo sawa na asilimia 162. Ongezeko la fedha za maendeleo limetoka na kupatiwa fedha za masoko shilingi bilioni 51,000,000,000 ambazo zilifanyiwa uhaulisho Serikalini **(Kiambatanisho nambari 3)**.

**Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu la Makao Makuu ya Afisi (D01)**

14. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa programu za Makao Makuu (D01) jumla ya Shilingi 33,936,200,000 ziliidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kati ya fedha hizo Shilingi 2,169,900,000 ni mishahara, Shilingi 3,628,700,000 ni matumizi mengineyo, Shilingi 28,000,000,000 ni kazi za maendeleo na Shilingi 137,600,000 ni Ruzuku kwa Tume

ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ. Hadi kufikia Machi 2024 Shilingi 63,930,214,042 zimepatikana sawa na asilimia 188 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,596,848,628 ni mishahara sawa na asilimia 74, Shilingi milioni 919,197,000 sawa na asilimia 25 ni matumizi mengineyo, Shilingi 61,348,516,014 sawa na asilimia 219 ni kazi za maendeleo na Shilingi 65,652,400 sawa na asilimia 48 ni ruzuku kwa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ.

**Upatikanaji wa Fedha kwa mafungu ya Idara Maalum za SMZ (D02-D06)**

15. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa programu zinazotekelezwa na mafungu matano ya Idara Maalum za SMZ (D02 – D06) yanayojumuisha Chuo cha Mafunzo (D02), Jeshi la Kujenga Uchumi (DO3), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (D04), Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (D05) na Kikosi cha Valantia Zanzibar (D06), kwa pamoja yaliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi 145,771,100,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 114,980,300,000 ni mishahara, Shilingi 18,311,400,000 ni matumizi mengineyo, Shilingi 479,400,000 ni ruzuku ya Wakala wa Ulinzi wa JKU na Shilingi 12,000,000,000 ni kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya Shilingi 107,997,782,164 zimepatikana sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka na asilimia 99 ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo Shilingi 90,340,615,963 sawa na asilimia 79 ni mishahara, Shilingi 12,699,101,076 sawa na asilimia 69 ni matumizi mengineyo, Shilingi 157,885,000 sawa na asilimia 33 ni ruzuku ya Wakala wa Ulinzi wa JKU na Shilingi 4,800,180,125 sawa na asilimia 40 ni kazi za maendeleo.

**Upatikanaji wa Fedha kwa Mikoa na Wilaya (D07-D11)**

16. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa programu zinazotekelezwa na mafungu matano ya Mikoa (D07-D11)

yanayojumuisha Mkoa wa Mjini Magharibi (D07), Mkoa wa Kusini Unguja (D08), Mkoa wa Kaskazini Unguja (D09), Mkoa wa Kusini Pemba (D10) na Mkoa wa Kaskazini Pemba (D11) jumla ya Shilingi 31,389,500,000 ziliidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 10,107,900,000 ni mishahara na Shilingi 3,078,100,000 ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Shilingi 20,460,683,189 zilipatikana sawa na asilimia 65 ya makadirio ya mwaka na asilimia 87 ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 6,653,756,577 sawa na asilimia 66 ni mishahara na Shilingi 1,260,325,000 sawa na asilimia 41 ni matumizi mengineyo.

**Upatikanaji wa Fedha za Ruzuku kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa**

17. **Mheshimiwa Spika,** kupitia mafungu matano ya Mikoa Baraza lako liliidhinisha ruzuku ya Shilingi 18,203,500,000 kutoka Serikali kuu kwenda kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya Shilingi 12,546,601,612 zilipatikana sawa na asilimia 69 ya makadirio ya mwaka na asilimia 85 ya makadirio ya miezi tisa. Fedha hizi za ruzuku zilitumika kulipa mishahara na shughuli za uendeshaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Upatikanaji wa Fedha kwa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii**

18. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (Fungu D12) liliidhinishiwa kutumia Shilingi 5,146,800,000 ambapo hadi kufikia Machi 2024, liliingiziwa Shilingi 2,638,138,293 sawa na asilimia 51 ya makadirio ya mwaka na asilimia 68 ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,635,300,00**0** sawa na asilimia 78 ni mishahara na Shilingi 592,235,878 sawa na asilimia 38 ni matumizi mengineyo.

## C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi imetekeleza na kuratibu miradi ya maendeleo ambayo imegawika katika maeneo makuu matatu. Maeneo hayo ni miradi ya maendeleo inayopatiwa fedha na Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar, miradi ya maendeleo inayopatiwa fedha na Washirika wa Maendeleo pamoja na miradi ya maendeleo inayopatiwa fedha zitokanazo na makusanyo ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

***Miradi Inayopatiwa Fedha na Tume ya Mipango Zanzibar***

**1) Mradi wa Kimkakati wa Ujenzi wa Masoko Makuu**

20. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea kusimamia ujenzi wa masoko ya kimkakati yanayojengwa Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini. Kwa upande wa soko la Mwanakwerekwe ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 98, Soko kuu la Jumbi ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 93 na Soko Kuu la Chuini na Stendi ya mabasi ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 80. Masoko haya yatakapozinduliwa na kuanza kutumika yatawanufaisha wajasiriamali 9,000 watakaokodishwa milango na vizimba vya kufanyia biashara zao. Kati ya wajasiriamali hao 5,000 watapatiwa nafasi Soko la Mwanakwerekwe, 2,500 watapatiwa nafasi Soko la Chuini na 1,500 watapatiwa nafasi Soko la Jumbi.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa malipo Mkandarasi wa Kampuni ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) inayojenga Soko la Mwanakwerekwe imeshawasilisha jumla ya *"certificate"* tano, Kampuni ya ujenzi ya Chuo cha Mafunzo inayojenga Soko la Jumbi imeshawasilisha "certificate" tano na Kampuni ya Ujenzi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi inayojenga soko la Chuini imeshawasilisha "certificate" sita. *"Certificates"* hizo zote nilizozitaja zimeshalipwa na Serikali

kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Hivyo basi, napenda kulitaarifu Baraza lako kuwa Serikali imeshalipa gharama za masoko haya kwa asilimia 100 kwa mujibu wa "certificates" zilizowasilishwa.

### 2) Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Masheha

22. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufanisi na uwajibikaji wa majukumu ya Waheshimiwa Masheha pamoja na kutoa huduma bora za kiutawala ngazi ya Shehia, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Afisi imefanikiwa kuanza ujenzi wa Ofisi 64 za Waheshimiwa Masheha ambapo Unguja zinajengwa jumla ya Ofisi 40 na Pemba zinajengwa jumla ya Ofisi 24. Ofisi hizi zinajengwa kwenye kila Wilaya Unguja na Pemba na Mkandarasi wake ni Kampuni ya Ujenzi wa Kikosi cha Valantia Zanzibar. Hadi kufikia Machi, Mkandarasi ameshalipwa malipo ya asilimia 30 ya ujenzi huo kwa mujibu wa mkataba. Aidha, Afisi imefanikiwa kupatiwa maeneo 150 yanayotarajiwa kujengwa Ofisi za Shehia awamu ya pili, kati ya maeneo hayo 83 ni Unguja na 67 Pemba ambapo zoezi la kuyapima na kuyahakiki maeneo hayo yaliyotengwa kujengwa ofisi za Waheshimiwa Masheha linaendelea kwa Unguja na Pemba. **(Kiambatanisho nambari 4)**

### 3) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama

23. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi imefanikiwa kutekeleza maeneo makuu manne ya mradi huu ambayo ni ununuzi wa vitendea kazi vya ulinzi, ununuzi na ufungaji wa vifaa vya mawasiliano ya ulinzi, ununuzi wa magari maalum ya shughuli za kiulinzi pamoja na utekelezaji wa usimamizi wa mradi wa Mji Salama. Lengo la utekelezaji wa mradi huu ni kutatua changamoto za Idara Maalum za SMZ katika utekelezaji wa majukumu yao ya kiulinzi. Utekelezaji wa mradi huu utasaidia kuimarisha hali ya usalama ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa wakati wote.

#### 4) Mradi wa Ujenzi wa Afisi, Nyumba na Mahanga

24. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa na Idara zote Maalum za SMZ ambazo ni Jeshi la Kujenga Uchumi, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, Chuo cha Mafunzo, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na Kikosi cha Valantia. Hatua za utekelezaji kwa kila Kikosi ni kama ifuatavyo;

a) Jeshi la Kujenga Uchumi limefanikiwa kujenga na kukamilisha Mahanga mawili na Afisi moja katika Kambi ya Chambani Pemba pamoja kuendeleza ujenzi wa jengo la Afisi ya Makao Makuu ya JKU Wawi Pemba ambapo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 75.

b) Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimekamilisha ujenzi wa Afisi ya Makao Makuu ya (KMKM) Wete Pemba pamoja na ujenzi wa Hanga, Afisi na kituo cha Afya katika Kambi ya Gando. Kwa upande wa Unguja Kikosi kimekamilisha ujenzi wa Afisi ya Makao Makuu ya Kamandi ya Kusini iliyopo Unguja Ukuu. Aidha, ujenzi wa Afisi ya Kamandi ya Kaskazini na hanga umefikia asilimia 90 katika Kambi ya Kibwengo.

c) Chuo cha Mafunzo kimekamilisha ujenzi wa jengo la Afisi ya Makao Makuu Wete Pemba pamoja na ujenzi wa Afisi ya Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo Kilimani Zanzibar ambapo ujenzi umefikia asilimia 77.

d) Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Afisi ya Zimamoto Mahonda Kanda ya Kaskazini Unguja pamoja na Hanga la Kulala Wapiganaji wa Zimamoto Finya Pemba. Kwa upande wa ujenzi wa nyumba za maafisa wa KZU Finya umefikia asilimia 55. Vile vile ujenzi wa msingi katika vituo vya Zimamoto na Uokozi Kiwengwa pamoja na Tasini Pemba unaendelea.

e) Kikosi cha Valantia kimekamilisha ujenzi wa nyumba mbili, Afisi na Hanga la kulala askari katika kambi ya

Mwanyanya na kukamilisha ujenzi wa nyumba nne na Afisi katika Kambi ya Mto wa Maji. Ujenzi wa Afisi, nyumba na hanga katika Kambi ya Kikungwi umefika asilimia 75 pamoja na ujenzi wa mahanga 4 ya kulala askari katika kambi ya Pangatupu umefikia asilimia 80.

### 5) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Usajili wa Matukio ya Kijami

25. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuimarisha mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii (CRVS) kwa kukamilisha mfumo wa kuunganisha wadau mbalimbali kuweza kuunganisha Mifumo yao kwa ajili ya kupata taarifa au kuhakiki taarifa wanazozihitaji. Uimarishaji huo wa mifumo umepelekea usajili wa ndoa na talaka kufanyika kwa njia ya mfumo wa kielektroni katika ngazi za Wilaya na kupelekea kuondosha usumbufu uliokuwa ukijitokeza awali kwa wananchi kufuata huduma hizo makao makuu ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## Miradi Inayopatiwa Fedha na Washirika wa Maendeleo

### 6) Mradi wa Kijani Pemba

26. **Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Kijani Pemba (Green & Smart Cities-SASA) unaotekelezwa na Jumuiya za Kimataifa ambazo ni OIKOS EAST AFRICA kwa Miji ya Wete na Micheweni na LIVIA kwa Miji ya Chake Chake na Mkoani unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), Ofisi imeratibu uzinduzi wa Kamati ya Usimamizi wa Mradi uliofanyika Kisiwani Pemba Tarehe14/11/2023. Aidha, Ofisi imeratibu upatikanaji wa Majengo ya Ofisi za Jumuiya hizo zilizopo Chake Chake na Wete. Mradi huu umejikita katika kusaidia upatikanaji wa huduma za maji safi na salama, usimamizi wa taka ngumu, mipango miji inayohusisha ukarabati wa Skuli, vituo vya afya na masoko pamoja na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

***Miradi Inayopatiwa Fedha za Makusanyo ya Ndani ya Serikali za Mitaa***

27. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na mambo mengine zina wajibu wa kuanzisha na kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inakwenda kutatua changamoto za wananchi kwenye maeneo yao. Katika utekelezaji wa matakwa hayo Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Unguja na Pemba zimetekeleza miradi ifuatayo;

a) Baraza la Manispaa Mjini linaendelea na kazi ya ufungaji wa taa 120 za mitaani katika wadi ya Kikwajuni, Rahaleo na Chumbuni ambapo hadi sasa jumla ya taa 60 zimeshafungwa.

b) Baraza la Manispaa Magharib "A" linaendelea na ujenzi wa Soko la KwaKisasi na Kituo cha Daladala Mndo ambapo Soko la KwaKisasi ujenzi umefikia asilimia 90 na Kituo cha Daladala Mndo ujenzi umefikia asilimia 75 ya utekelezaji. Aidha, Baraza limenunua kwa njia ya mkopo gari kubwa tatu za kuzolea taka na kijiko kimoja kwa lengo la kupunguza kadhia ya uwepo wa taka katika Manispaa ya Magharib "A"

c) Baraza la Manispaa Magharib "B" limekamilisha uwekaji wa taa 21 za mitaani katika wadi ya Jitimai na kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Polisi Fuoni Kipungani ambao upo katika hatua ya kuezeka paa.

d) Baraza la Mji Kati limekamilisha ujenzi wa Soko la Mazao ya Baharini Kikungwi na kutoa ruhusa ya wajasiriamali akina mama waliokuwa wakiuza mazao ya baharini pembezoni mwa Barabara kuu kuingia kwenye soko hilo kuendeleza shughuli zao za biashara. Vile vile, Baraza limekamilisha ujenzi wa vituo 10 vya kusubiria Daladala kwa lengo la kuwaondoshea adha wananchi katika kipindi cha jua na mvua.

e) Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imekamilisha kutekeleza mradi wa Kituo kikuu cha Daladala Michamvi. Vilevile, Halmashauri imekamilisha kufanya ununuzi wa pembea kwa ajili ya kiwanja cha kufurahishia watoto Paje na kukamilisha ujenzi wa Soko la Kizimkazi awamu ya kwanza.

f) Baraza la Manispaa Kaskazini "A" linaendelea na mradi wa ujenzi wa Soko la Mkwajuni na Chaani ambapo ujenzi wa soko la Mkwajuni umefikia asilimia 70 na ujenzi wa soko la Chaani umefikia asilima 55.

g) Baraza la Mji kaskazini "B" limefanikiwa kukamilisha ujenzi wa mradi wa soko la Donge Mtambile na mradi wa soko la Kitope umefikia asilimia 70. Ujenzi wa vituo vinne vya kusubiria daladala katika maeneo ya Mahonda, Kinduni, Mgambo na Kiwengwa umekamilika.

h) Baraza la Manispaa Chake Chake, limekamilisha kutekeleza mradi wa Soko la Machomanne na mradi wa ujenzi wa kituo cha kusubiria abiria katika Hospitali ya Wilaya ya Vitongoji. Aidha, ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi umefikia asilimia 75 pamoja na ujenzi wa maegesho ya gari Tibirinzi upo katika asilimia 80.

i) Baraza la Mji Mkoani limekamilisha ujenzi wa Soko la Mtambile pamoja na kufanya matayarisho ya ujenzi wa soko la Kengeja.

j) Baraza la Mji Wete, limejenga vituo sita (6) vya kusubiria daladala katika maeneo ya Raha, Jumapili Kiuyu, Bahanasa njia ya Mtambwe, Kiyapaka Mtambwe, Kizimbani na Gando. Pia Baraza limekamilisha ujenzi wa msingi wa maji ya mvua pamoja na uwekaji sawa wa ardhi (landscaping) katika eneo la Soko la Wajasiriamali Kifumbikai.

k) Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imekamilisha kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Stendi ya kisasa ya Kinowe Konde ambayo imeanza kutoa huduma kwa wananchi.

28. **Mheshimiwa Spika,** kwa pamoja Mamlaka Serikali za Mitaa zimeendelea kusimamia na kutekeleza miradi mbalimbali ya Wadi katika sekta za maji, elimu na miundombinu.

## D. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA PROGRAMU ZA IDARA ZA MAKAO MAKUU YA AFISI

29. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya programu tatu zinatekelezwa ngazi ya Makao Makuu ya Wizara kupitia Idara za ndani. Programu hizo ni Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Programu ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ na Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi. Katika utekelezaji wa programu hizo miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo;-

### 1) Kuwapatia Waheshimiwa Masheha vitendea kazi muhimu

30. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufanisi na uwajibikaji wa majukumu ya Waheshimiwa Masheha pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi, Serikali kupitia Afisi hii imefanikisha zoezi la kuwapatia Masheha wote 388 Bendera za Serikali ambazo zinatambulisha utawala wa Serikali ngazi ya Shehia. Aidha, Serikali imekamilisha zoezi la kumpata Mzabuni ambaye ni Wakala wa Uchapaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutengeneza mihuri ya kisasa kwa ajili ya kuwapatia Masheha ili kuepukana na hatari ya watu wasio waaminifu kutaka kughushi mihuri ya Waheshimiwa Masheha. Hadi kufikia sasa jumla ya Waheshimiwa Masheha121 tayari wameshapatiwa mihuri hiyo ya kisasa na wameanza kuitumia.

### 2) Kupandishwa hadhi Mabaraza ya Miji kuwa Manispaa

31. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia ukuaji wa shughuli za kiuchumi na huduma za miundombinu ya kijamii katika Wilaya za Kaskazini “A” na Chake Chake, Serikali imefanya maamuzi

ya kuyapandisha hadhi yaliyokuwa Mabaraza ya Miji ya Kaskazini ''A'' na Chake Chake kuwa Mabaraza ya Manispaa. Kupandishwa hadhi huko kumepelekea sasa Zanzibar kuwa na Mabaraza matano ya Manispaa yaliyopo katika Mikoa mitatu kati ya Mikoa mitano tuliyonayo. Aidha, upandishaji huo wa hadhi unapelekea Manispaa zetu kuwa na uwezo wa kukabiliana na kasi ya ukuwaji wa miji na utoaji wa huduma kwa wananchi.

### 3) Kupandishwa Vyeo Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ

32. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imewapandisha vyeo Maafisa na Wapiganaji 2,652 (wanawake 547 na wanaume 2,105) wa Idara Maalum za SMZ kutokana na utendaji na uzoefu wao wa kazi. Kati ya Maafisa wa ngazi za juu 60 (wanaume 39 na wanawake 21) wamepandishwa vyeo na Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

33. **Mheshimiwa Spika**, Maafisa wa ngazi ya kati 148 (wanawake 57 na wanaume 91) wamepandishwa vyeo na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ. Aidha, Wapiganaji 2,444 (wanawake 469 na wanaume 1,975 ) wamepandishwa vyeo na Wakuu wa Idara Maalum za SMZ kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ. Upandishwaji wa vyeo kwa Maafisa na Wapiganaji katika utumishi wa kijeshi ni sehemu muhimu ya kuboresha utendaji wao wa kazi na maslahi yao ambapo pia kunaimarisha shughuli za ulinzi na usalama nchini. **(Kiambatanisho nambari 5)**

### 4) Kuzipatia Hati Miliki Kambi za Idara Maalum za SMZ

34. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imetoa hatimiliki tisa za matumizi ya ardhi kwa Kambi nne za Kikosi cha Valantia (KVZ), Kambi tatu za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), na Kambi moja moja kwa

Chuo cha Mafunzo na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Vile vile, Afisi imeshalipa upatikanaji wa hatimiliki wa Kambi sita ambazo Kambi tatu ni kwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na tatu ni za Chuo cha Mafunzo. Aidha, Afisi imeshafanya malipo ya kupimiwa maeneo ya Kambi nane ambazo sita ni za Kikosi cha Zimamoto na mbili za Kikosi cha KMKM. Lengo la upimaji na upatikanaji wa hati ni kuzilinda kambi za Idara Maalum za SMZ na kuepusha migogoro baina ya wananchi na vyombo vyetu vya ulinzi.

**5) Kuboreshwa kwa Miundombinu ya Viwanda vya Idara Maalum za SMZ**

35. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeboresha miundombinu ya viwanda vya Idara Maalum za SMZ ambapo jumla ya vyarahani vipya 123 vya kisasa vimenunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya Kiwanda cha Ushoni wa Nguo. Vilevile, jumla ya mashine mpya 21 za kisasa za Kiwanda cha viatu pamoja na mashine mbili mpya za kutengenezea mifuko isiyo ya plastiki zimenunuliwa. Viwanda vya Idara Maalum za SMZ kwa sasa vina uwezo wa kutengeneza aina mbali mbali za nguo, viatu, mifuko, mabango (banners) na kutengeneza Bendera za Serikali.

**6) Ziara ya Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ Vikosini**

36**. Mheshiwa Spika,** Afisi imeratibu ziara ya Kamanda Mkuu wa Idara Maalum za SMZ ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi iliyofanyika kwa kutembelea Idara Maalum zote za SMZ siku ya tarehe 9/3/2024 na tarehe 10/3/2024. Lengo la ziara hiyo ni kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili maafisa na wapiganaji, changamoto zinazokabili utendaji, kuhimiza nidhamu na uwajibikaji pamoja na kuelezea maboresho yanayofanywa na Serikali kwa maendeleo ya Idara Maalum za SMZ.

### 7) Kuimarishwa kwa Jumuiya zisizo za Kiserikali Zanzibar (NGOs).

37. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuimarisha maendeleo ya Jumuiya zisizo za Kiserikali nchini. Mchango wa Jumuiya hizo katika kusaidia shughuli mbali mbali za kimaendeleo Zanzibar umeongezeka kwa asilimia 19 kutoka Shilingi bilioni 49 kwa mwaka fedha 2022/2023 na kufikia Shilingi bilioni 58 hadi Machi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, Jumla ya Shilingi 47,332,619,465 zimepatikana kwa NGOs 145 za Unguja na Shilingi 11,643,095,665 kwa NGOs 21 za Pemba. Aidha, Serikali imefanikiwa kusajili Jumuiya 103, kati ya hizo jumuiya 80 Unguja na Jumuiya 23 Pemba baada ya kukidhi masharti yaliyowekwa kisheria. **(Kiambatanisho nambari 6)**

### 8) Kufanyika kwa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria za Idara Maalum za SMZ

38. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya marekebisho mbali mbali ya Sheria zote za Idara Maalum za SMZ kwa lengo la kuziwezesha Idara hizo kufanya shughuli za kiuchumi na kimaendeleo kwa ufanisi na kwa mujibu wa sheria. Marekebisho hayo tayari yameshatoka Serikalini na hatua inayofuata ni kuwasilishwa katika Baraza lako Tukufu.

## E. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ

39. **Mheshimiwa Spika,** Idara Maalum za SMZ zinatekeleza programu kuu 10 ambapo kila Kikosi kimepangiwa kutekeleza programu kuu mbili. Katika utekelezaji wa programu hizo mafanikio yafuatayo yamepatikana ambayo yamewezesha kuimarisha hali ya ulinzi na usalama nchini.

### 1) Kutoa Malezi ya Vijana kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)

40. **Mheshimiwa Spika,** programu ya malezi kwa vijana inatekelezwa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) chini ya kifungu

cha nne (a) cha Sheria nambari 06 ya Mwaka 2003, Sheria za Zanzibar. Kwa mwaka fedha 2023/2024 jumla ya vijana 1,680 kutoka Mikoa yote ya Zanzibar walikidhi vigezo na sifa za kujiunga na mafunzo ya ujenzi wa Taifa mkupuo 070 yanayotolewa na JKU. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaandaa vijana wa Zanzibar katika shughuli za kiuchumi na uzalishaji mali ili waweze kujitegemea pamoja na kuwajenga kuwa wazalendo wa Taifa lao.

41. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2024, JKU ina jumla ya vijana 8,476, kati yao vijana 4,546 (wanawake 812 na wanaume 3,734) wanapatiwa mafunzo ya ujenzi wa Taifa katika shughuli za uzalishaji mali kwenye kilimo, uvuvi na ufugaji. Vijana 2,467 (wanawake 592 na wanaume 1,875) wanapatiwa mafunzo ya elimu ya ufundi katika stadi mbali mbali zitolewazo na Skuli ya Ufundi JKU Mtoni. Aidha, vijana 1,456 (wanawake 796 na wanaume 660) wanapatiwa mafunzo ya elimu ya sekondari katika mchipuo wa sayansi katika Skuli ya Sekondari ya JKU Mtoni.

**2) Kusimamia misingi ya haki jinai Chuo cha Mafunzo**

42. **Mheshimiwa Spika,** katika usimamizi wa haki jinai nchini kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024 kupitia programu ya urekebishaji tabia, jumla ya wanafunzi na mahabusu 1,193 waliamriwa na Mahkama kwenda Chuo cha Mafunzo. Kati yao wanafunzi 296 (Unguja 206 na Pemba 90) na mahabusu 897 (Unguja 681 na Pemba 216). Aidha, wanafunzi 142 (wanaume 138 na wanawake wanne 4) wameruhusiwa baada ya kumaliza mafunzo yao ambapo pia wanafunzi 25 wote wanaume wamepata msamaha wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kwa mnasaba huo, Chuo cha Mafunzo hadi kufikia machi 2024 kina wanafunzi 678 ambapo kwa Unguja ni 526 na Pemba ni 152.

43. **Mheshimiwa Spika**, hali ya idadi ya wanafunzi na mahabusu wa Chuo cha Mafunzo ni kubwa ikilinganishwa na miundombinu ya eneo la Kiunua Miguu Kilimani. Changamoto hii imepelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuja na Mpango Mkakati mpya wa kuimarisha haki za jinai nchini kwa kuamua kujenga Chuo cha Mafunzo kipya Hanywegwa Mchana, mpango ambao utatekelezwa katika bajeti ya mwaka 2024/2025.

**3) Ulinzi wa bahari, udhibiti wa magendo na uokozi baharini**

44. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimefanikiwa kufanya ulinzi katika eneo la bahari ya Zanzibar ili kuzuia uharibifu unaoweza kufanywa dhidi ya rasilimali za bahari. Jumla ya doria 84 zimefanyika ambapo doria 51 zimefanyika baharini na doria 33 zimefanyika nchi kavu. Katika doria hizo, matukio 57 ya usafirishaji wa magendo yameweza kudhibitiwa ikiwemo matukio 20 ya usafirishaji wa magendo ya karafuu.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika kutoa huduma ya uokozi baharini, Kikosi cha KMKM kimefanikiwa kuwaokoa wananchi 257 waliokuwa wakijishughulisha na shughuli mbali mbali za uvuvi na usafiri ambapo wananchi 226 waliokolewa wakiwa hai na wananchi 31 wakiwa wameshapoteza maisha. Naomba kutoa wito kwa wananchi wanaotumia bahari kufuata maelekezo na hadhari zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa lengo la kunusuru uhai wa maisha yao na mali zao. Kadhalika, nawaomba wananchi kutumia vyombo imara vinavyohimili mawimbi ya bahari wakiwa katika shughuli zao.

**4) Kutoa huduma za zimamoto kwenye maeneo mbali mbali**

46. **Mheshimiwa Spika,** huduma za zimamoto zimeendelea kutolewa katika maeneo mbali mbali yaliyoripotiwa katika

Vituo vya Zimamoto Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, jumla ya matukio ya moto 193 yaliripotiwa na kuchukuliwa hatua stahiki ikiwemo kuzima moto usiendelee kuleta athari, uokozi wa watu na mali zao. Kati ya matukio hayo, matukio 131 yalihusisha moto kwenye nyumba za makaazi na majengo ya taasisi, matukio 22 yalihusisha moto wa vyombo vya usafiri barabarani, matukio 19 ni moto wa mashambani, matukio 15 ni moto sehemu za maduka na matukio 6 ni moto wa ndege katika viwanja vya ndege. Matukio hayo yamesababisha hasara ya Shilingi bilioni 6.15 kwa mujibu wa ripoti ya tathmini zilizofanywa na Kikosi.

**5) Kuimarisha huduma za zimamoto katika viwanja vya ndege**

47. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuimarisha huduma za zimamoto kwenye viwanja vya ndege kwa kufanya matengenezo makubwa ya gari za zimamoto ziliopo kwenye viwanja vya ndege. Vile vile, Serikali imeweza kuongeza nguvu ya idadi ya maafisa na askari wa zimamoto pamoja na kuwapatia mafunzo maalum ya kukabiliana na ajali za moto katika viwanja vya ndege. Aidha, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeingia makubaliano (MoU) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) yenye lengo la kupunguza mzigo uliokuwa unabebwa na KZU kwenye viwanja vya ndege na kuongeza ufanisi wa shughuli za KZU katika viwanja vya ndege. Hivyo, makubaliano hayo yanapelekea kuanzia sasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwa na jukumu la kununua gari za zimamoto, kufanya matengenezo ya gari hizo, kununua mafuta, kununua dawa za kuzimia moto pamoja na kutoa mafunzo kwa Wapiganaji wa zimamoto. Lengo likiwa ni kuboresha huduma za zimamoto katika viwanja vya ndege hususan Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA).

### 6) Kupambana na makundi ya kihalifu na kuimarisha ulinzi nchini

48. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya ulinzi wa raia na mali zao Kikosi cha Valantia kimeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kisheria kwa kufanya operesheni maalum katika maeneo mbali mbali yaliyoripotiwa kujitokeza makundi yaliyokuwa yakihatarisha usalama wa wananchi na mali zao. Kufuatia operesheni hizo, watuhumiwa 28 walikamatwa na kukabidhiwa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua za kufikishwa Mahakamani. Aidha, operesheni hizo zimelenga kuimarisha hali ya usalama wa wananchi na mali zao katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi cha Valantia kimeendelea kutoa huduma za ulinzi kwa majengo ya Ofisi za Serikali na nyumba za Viongozi wa Serikali. Kadhalika, Kikosi kimeshirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini kufanikisha shughuli mbali mbali za ulinzi. Aidha, kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania, Kikosi kimepatiwa mafunzo ya kijeshi yaliyolenga kuimarisha ulinzi wa nchi na mipaka yake.

### 7) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa na Wapiganaji

50. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanikiwa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kijeshi Maafisa na Wapiganaji 1,121 wa Idara Maalum za SMZ. Kati yao, Wapiganaji 457 (wanaume 381 na wanawake 76) wamepatiwa mafunzo ya uongozi mkubwa na Wapiganaji 508 (wanaume 392 na wanawake 116) wamepatiwa mafunzo ya uongozi wa kati. Mbali na mafunzo hayo ya kijeshi, maafisa na Wapiganaji 156 (wanaume 115 na wanawake 41) wameendelezwa kitaaluma katika vyuo vikuu mbali mbali nchini kwa mujibu wa fani husika. Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuimarisha utendaji wa Idara Maalum za SMZ kwa kuwajengea uwezo maafisa na wapiganaji kufanya kazi zao kwa uweledi na ujuzi. **(Kiambatanisho nambari 7)**

### 8) Kutoa huduma za Afya kwa Maafisa, Maaskari na Wananchi

51. **Mheshimiwa Spika,** huduma za afya zimeendelea kutolewa kwa Maafisa, Maaskari na Wananchi kupitia Kambi mbali mbali za Idara Maalum zilizopo Unguja na Pemba. Jumla ya wagonjwa 139,355 (wanawake 80,823 na wanaume 58,532) wamepatiwa matibabu katika hospitali ya KMKM Kibweni na Vituo vya Afya vilivyopo katika Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Uchumi Saateni, Chuo cha Mafunzo Kilimani na Kikosi cha Valantia Mtoni.

52. **Mheshimiwa Spika,** kambi za matibabu za maradhi mbalimbali zimefanyika kupitia Vikosi vya KMKM na JKU. Kwa upande wa KMKM walishirikiana na madaktari kutoka Ujerumani kutoa matibabu ya macho ambapo wananchi 520 walifanyiwa upasuaji wa macho. Aidha, KMKM kwa kushirikiana na madaktari kutoka Marekani walitoa matibabu ya vidonda sugu kwa wananchi 20. Kwa upande wa JKU waliendesha kambi nne za matibabu ya pua na koo ambapo jumla ya wananchi 85 walifanyiwa upasuaji

### 9) Uzalishaji wa mazao ya kilimo na ufugaji

53. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kuimarisha shughuli za uzalishaji wa kilimo na ufugaji kwenye Jeshi la Kujenga Uchumi na Chuo cha Mafunzo. Uzalishaji huu kwa Chuo cha Mafunzo na JKU umesaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza utegemezi wa chakula na kuimarika kwa huduma zinazohitaji chakula katika taasisi hizo.

### 10) Ushiriki wa Idara Maalum katika Michezo

54. **Mheshimiwa Spika,** timu za Idara Maalum zote za Wanawake na Wanaume zimefanikiwa kushiriki katika michezo mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo mashindano ya Majeshi Tanzania (BAMATA), riadha, mpira wa wavu, kuogelea, judo

na wameonyesha kiwango cha juu cha kiushindani katika michezo hiyo.

55. **Mheshimiwa Spika,** sote ni mashahidi timu za Idara Maalum za SMZ hususan za mpira wa miguu zimeendelea kuwa na mchango mkubwa katika uimarishaji wa michezo na kielelezo kikubwa ni ligi kuu ya Zanzibar. Michezo hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga afya za Wapiganaji na kuwa na utayari wa kulinda amani ya nchi yetu muda wote.

## F. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA TAWALA ZA MIKOA

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Mikoa imetekeleza Programu tatu ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Serikali katika Mikoa, Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Mikoa na Wilaya na Programu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa. Katika utekelezaji huu, mafanikio yafuatayo yamepatikana;

### 1) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za kisekta katika Mikoa

57. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa programu ya kuratibu shughuli za Serikali Mikoani na Wilayani, Ofisi za Waheshimiwa Wakuu Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kushirikiana na viongozi na watendaji wa sekta mbalimbali za Serikali wameratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli mahsusi za kisekta kwa lengo la kuhakikisha huduma zote muhimu za Serikali zinawafikia wananchi popote pale walipo. Miongoni mwa sekta zilizoratibiwa ni Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu, Sekta ya Kilimo, Sekta ya Maji na Nishati, Sekta ya Uwekezaji, Sekta ya Uwezeshaji, Sekta ya Biashara, Sekta ya Michezo, Sekta ya Miundombinu na Sekta za masuala mtambuka.

### 2) Usimamizi wa Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Udhalilishaji

58. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya jitihada mbalimbali zimeendelea

kuchukuliwa za kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Aidha, vikao mbali mbali vya wadau wanaopinga vitendo vya udhalilishaji vimekaliwa kwa lengo la kuandaa mikakati ya kupunguza matukio hayo kwenye jamii na kuimarisha hifadhi ya wanawake na watoto ikiwemo kuhamasisha wananchi kuripoti katika vyombo vya sheria mara tu yanapotokea matukio hayo. Vile vile, Mikoa imeshirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike yaliyofanyika 10/10/2023, Siku ya Mtoto Duniani iliyoadhimishwa tarehe 20/10/2023 na Siku ya Mwanamke iliyoadhimishwa tarehe 08/03/2024.

### 3) Kusimamia na kudumisha Amani, Utulivu na Mshikamano

59. **Mheshimiwa Spika,** Mikoa imeendelea kusimamia jukumu lake la msingi la ulinzi na usalama kwa kuhakikisha masuala ya uwepo wa amani, utulivu na mshikamano yanadumishwa muda wote ili kuwawezesha wananchi na wageni wetu kufanya shughuli zao za kimaendeleo. Jumla ya vikao 159, kati ya hivyo vikao vya kawaida 100 na 59 vya dharura vya Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya vilifanyika. Vikao hivyo vilijadili mambo mbali mbali kama vile vitendo vya mauaji, wizi wa kutumia nguvu, uwepo wa bandari bubu zinazotumika kusafirisha magendo, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya, ajali za barabarani, vitendo vya udhalilishaji pamoja na kujadili juu ya kufanya operesheni za kupambana na matukio yanayochochea uvunjifu wa amani, utulivu na mshikamano.

60. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia vikao hivyo vya Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya, operesheni maalum za kushtukiza zilifanyika na kufanikiwa kukamata matukio mbalimbali kama vile madawa ya kulevya, vitendo vya uvunjifu wa amani. Operesheni hizo zililenga kuzuia

baadhi ya matukio yasitokee na kupambana na matukio yaliyojitokeza ili kunusuru athari zake kutokuenea katika jamii. **(Kiambatanisho nambari 8)**

**4) Kupambana na wizi wa mazao na mifugo.**

61. **Mheshimiwa Spika,** Jitihada za kupambana na wizi wa mazao na mifugo katika jamii zimeendelea kufanyika kupitia Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambapo Mikoa imefanya mikutano mbalimbali katika ngazi ya shehia kuhamasisha wananchi kukata vibali vya kusafirishia mazao na mifugo. Aidha, Mikoa imefanya operesheni na kufanikiwa kukamata mifugo ya ng'ombe waliokuwa wameibiwa katika maeneo mbalimbali wakiwa hai na wengine wakiwa wamechinjwa. Kwa ujumla kufuatia operesheni hizo jumla ya watu 68 walikamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya wizi wa mazao na mifugo.

**5) Usuluhishi wa Migogoro ya ardhi.**

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuchukua hatua dhidi ya migogoro ya ardhi inayojitokeza katika jamii. Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi wamesuluhisha migogoro 61 kati ya migogoro 177 iliyoripotiwa kwenye ofisi za Mikoa na Wilaya. **(Kiambatanisho nambari 9)**

**6) Uratibu wa Ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Mikoa**

63. **Mheshimiwa Spika,** Mikoa imeendeleza jukumu lake la kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Katika ziara hizo Mikoa yote mitano imebahatika kutembelewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi. Aidha, Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza

na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili nao wamefanya ziara katika Mikoa yote ya Zanzibar.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya ziara katika Mikoa ya Kusini Unguja, Kusini Pemba, Kaskazini Unguja na Mkoa wa Mjini Magharibi. Mheshimiwa Dkt. Philip Isidori Mpango Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya ziara katika Mkoa wa Kusini Unguja wakati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano amefanya ziara katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

65. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia ziara za Viongozi wetu wa Kitaifa, ahadi, maagizo na maelekezo mbalimbali yametolewa ambapo ofisi za Mikoa zinaratibu utekelezaji wake na kuwasilisha katika Mamlaka husika. Ziara hizo kwa hakika zimekuwa na tija na zinafurahiwa na wananchi kwa kuwa zinaleta suluhu ya changamoto zao.

## G. MAFANIKIO YA PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERIKALI ZA MITAA

### 1) Kusimamia Usafi wa Mazingira

66. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha usafi wa mazingira kwa kuondosha taka na kupelekwa katika majaa makuu likiwemo jaa la Kibele Unguja na Vitongoji Pemba. Operesheni za usafishaji wa majaa rasmi na yasiyo rasmi zimefanyika katika Manispaa za Jiji la Zanzibar, pamoja na kufanya usafi wa mitaro ya maji ya mvua, maji machafu na usafi wa barabara kuu.

67. **Mheshimiwa Spika,** zoezi la ukaguzi wa mazingira katika maeneo ya makaazi na biashara limefanyika katika Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote za Unguja

ambapo jumla ya maeneo 31,855 ya makaazi na biashara yamekaguliwa. Lengo la ukaguzi huo ni kuimarisha mfumo salama wa makaazi na kulinda afya za wananchi na wageni. Aidha, zoezi la utoaji wa elimu kwa jamii juu ya usafi wa mazingira kwenye maeneo yao limefanyika kupitia mikutano mbalimbali katika ngazi ya Shehia na vipindi 47 vya redio na televisheni vilivyoandaliwa na kurushwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar.

68. **Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa shughuli za usarifu wa taka ngumu, Serikali kupitia Baraza la Jiji limejenga kituo maalum cha kuhifadhi na kusarifu taka ngumu katika Wadi ya Chumbuni kwa lengo la kuzibadilisha taka zinazooza kuwa mbolea na chakula cha kuku. Vile vile, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeviwezesha vikundi vya shehia vinavyojihusisha na usafi wa mazingira kufundishwa namna ya kutengeneza mkaa, mbolea, vigae na matofali pamoja na kupewa elimu ya biashara na utafutaji wa masoko ya bidhaa zitokanazo na taka ili kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao.

69**. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya kufanyia usafi Baraza la Manispaa ya Magharibi ‘’A”limenunua jumla ya gari tatu za kubebea taka pamoja na gari la kijiko cha kuzolea taka kwa njia ya mkopo uliotolewa na Benki ya Amana Tawi la Zanzibar. Aidha, Baraza la Manispaa ya Mjini limepokea msaada wa mapipa 90 ya kuhifadhia taka yenye ujazo wa lita 250 na mabero 50 kutoka Ubalozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China. Vile vile, Serikali inatarajia hivi karibuni kulipatia Baraza la Manispaa ya Mjini vikapu vipya vya taka (kontena) 65 ili kuimarisha usafi katika eneo letu la Mjini.

**2) Kujenga mahusiano baina ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar na Taasisi za nje ya Zanzibar.**

70. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanikiwa kujenga mahusiano na mashirikiano na taasisi za nje ya Zanzibar kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika maeneo mbali mbali ya kiutendaji. Kwa mfano Baraza la Jiji limefanya mashirikiano na Taasisi ya AATRADEX ZURICH CONSULTANT ya Switzerland, Jumuiya ya Serikali za mitaa Afrika ya Mashariki (EALGA), Umoja wa Majiji na Serikali za Mitaa Afrika (UCLGA) pamoja na Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania Bara (ALAT). Mahusiano na mashirikiano hayo yamepelekea Mkutano Mkuu wa 38 wa ALAT kufanyika kwa mara ya kwanza Zanzibar kwa kushirikiana na Jumuiya ya Serikali za Mitaa Zanzibar (ZALGA).

71. **Mheshimiwa Spika,** mashirikiano ya udugu baina ya Manispaa ya Mjini na Jiji la Potsdam la Ujerumani yanaendelea vizuri na kwa sasa utekelezaji wa Mradi wa "Biocooling" unaendelea wenye lengo la kuimarisha haiba ya kijani na kupunguza ongezeko la joto mjini linalosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi. Kupitia mradi huo jumla ya miti 2,350 imepandwa katika maeneo ya Mtoni Kidatu, Botanic Garden (Migombani) na Maruhubi. Sambamba na hilo Baraza la Manispaa ya mjini limefungiana mkataba wa udugu na Manispaa ya Mamadou ya Mauritius. Aidha, Baraza la Jiji Zanzibar limeingia makubaliano ya udugu na Jiji la Weihai katika jimbo la Shading la nchini China.

**3) Kuchangia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi**

72. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetekeleza jukumu lake la kisheria la kuwasilisha mchango wa asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kusaidia wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Jumla ya Shilingi 746,395,835 zimewasilishwa katika mfuko wa uwezeshwaji wananchi kiuchumi. Aidha, Mamlaka za

Serikali za Mitaa zimefanya vikao vya pamoja na Wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi (ZEEA) kujadiliana juu ya namna bora ya kuwasilisha fedha hizo na kuwafikia walengwa.

## H. MAFANIKIO YA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

### 1) Kushusha Usajili wa Matukio Yote ya Kijamii Wilayani

73. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kusajili matukio ya kijamii mbalimbali kupitia Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii zilizopo kila Wilaya Unguja na Pemba. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa kwenye Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (CRVS) ambayo yamepelekea usajili wa ndoa na talaka kufanyika kielektroniki ambapo awali haukua ukifanyika kielektroniki. Hatua hii kunaifanya Serikali kukamilisha kushusha usajili wa matukio yake yote ya kijamii katika ngazi za Wilaya.

### 2) Mifumo ya Usajili Kusomana na Mifumo Mingine

74. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuboresha mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii (CRVS) kwa kuuwekea mlango (Stakeholders Gateway). Maboresho haya sasa yanauwezesha mfumo huu kuweza kuzungumza na mifumo mingine mbali mbali ukiwemo mfumo wa vitambulisho vya Kitaifa.

### 3) Kuweka Ulinzi na Usalama wa Mifumo ya Usajili

75. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeandaa mpango wa huduma endelevu (Business Continuity plan) na mpango wa urejeshaji wa huduma (Disaster recovery plan) wakati wa majanga ili kuweka ulinzi na usalama wa mifumo. Kwa kuwa sasa huduma zote za usajili zinatumia mifumo ya usajili ya kielektroniki, Serikali imeona ipo haja ya kuwa na mipango miwili iliyotajwa ili kuhakikisha kuwa, huduma zinapatikana muda wote na pale yanapotokea majanga na kuathiri mifumo

husika, zinakuwepo njia za kuondoa athari, kurejesha mifumo pamoja na taarifa kama ilivokuwa awali.

## I.MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itaendelea kutekeleza Programu Kuu 18 kupitia Mafungu 12 yaliyoanzia D01 hadi D12. Fungu D01 (Makao Makuu) limepangiwa kutekeleza programu kuu tatu; Mafungu matano ya Idara Maalum za SMZ (D02–D06) yatatekeleza programu kuu 10; Mafungu matano ya Mikoa (D07-D11) yatatekeleza programu kuu tatu na Fungu la Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii (D12) litatekeleza programu kuu mbili.

## J. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA MAKAO MAKUU (D01)

77. **Mheshimiwa Spika,** Afisi kupitia fungu la bajeti la Makao Makuu chini ya Idara za Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ, Afisi Kuu Pemba, Afisi ya Mrajisi wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali pamoja na Viwanda vya Idara Maalum za SMZ imepanga kutekeleza malengo yafuatayo kwa mwaka fedha 2024/2025;-

a. Serikali imepanga kuanza ujenzi wa Mradi wa Kituo cha Mabasi ya Kisasa na Maegesho katika eneo la Bwawa la Mwanakwerekwe ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

b. Serikali imekusudia kuhamisha Chuo cha Mafunzo Kiinua Miguu kwa kuanza kujenga Chuo kipya cha kisasa Hanyegwa mchana ambacho kitakuwa na uwezo wa kubeba

wanafunzi wasiopungua 1000 na mahabusu wasiopungua 1000 pamoja na miundombinu mengine. Hatua hiyo ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara 204 (f) kwa mwaka 2020-2025. Aidha, hatua hiyo ni utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c. Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar ambao umelenga kuziimarisha Idara Maalum za SMZ kwa kuzipatia vifaa vya kisasa vya kiulinzi na mafunzo zaidi ya kiulinzi katika kutekeleza jukumu la kuimarisha ulinzi na usalama wakati wote nchini.

d. Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Masheha awamu ya pili ili kuimarisha utendaji wao na kuruhusu kupatiwa kibali cha ajira za Makatibu wa Masheha kwa maeneo ambayo ofisi hizo zitakuwa zimekamilika na kuzinduliwa kwa matumizi.

e. Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Pemba Kijani unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya kwa Miji ya Chake Chake, Mkoani, Wete na Micheweni. Mradi huu lengo lake ni kuwawezesha Wananchi wa Miji hiyo kupata huduma muhimu zitokanazo na kasi ya ukuaji wa Miji na uhamiaji wa wananchi mijini (Urban migration).

f. Kuyazindua na kuanza kuyatumia masoko makuu ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini ikiwa pamoja na kuwapanga Wajasiriamali kwenye Masoko hayo ili wasifanye biashara zao katika maeneo yasiyo rasmi na maeneo ya barabarani.

g. Kufanya ukarabati mkubwa wa Jengo la Afisi Kuu ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba, ili kuendana na hadhi ya Ofisi za Umma na kujenga mazingira bora ya kazi kwa Afisa Mdhamini na watendaji wengine.

h. Kuzipatia Mamlaka za Serikali za Mitaa vifaa vya kisasa vya usafi wa mazingira ikiwemo magari kwa njia ya mkopo pamoja na kuruhusu sekta binafsi kutoa huduma za usafi wa mazingira (outsourcing). Aidha, Afisi itaandaa Mpango Mkuu wa Usafi wa Majitaka Zanzibar na mpango mkuu wa usafi wa taka za vifaa vya umeme.

i. Kuzindua na kuanza kutumia mfumo mpya wa kielektroniki wa taarifa za ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ujulikanao kwa jina la ZAN-MUTM. Mfumo huo utasaidia kwa kiasi kikubwa udhibiti wa uvujaji wa mapato na kuyatumia mapato hayo kutoa huduma bora kwa wananchi.

j. Kuimarisha usajili na uratibu wa Jumuiya zisizo za Kiserikali Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha Jumuiya zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria za Nchi sambamba na kuhakikisha wananchi wananufaika na Jumuiya hizo.

k. Kuboresha huduma za uzalishaji wa viwanda vya Idara Maalum za SMZ kwa kuhakikisha Viwanda vinazalisha bidhaa bora zenye kuleta ushindani katika Soko. Aidha, Viwanda vitaimarishwa kwa kuhakikisha mahitaji ya Idara Maalum za SMZ yanapatikana kwa wakati.

l. Kuimarisha mfumo wa mafunzo kwa Idara Maalum za SMZ na kuzidisha operesheni za kuimarisha ulinzi na usalama kwa kushirikiana na vyombo vengine vya ulinzi vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

m. Kuanzisha mchakato wa upandishwaji hadhi Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja na Halmashauri ya Wilaya Micheweni kwa kuzingatia vigezo vya kisheria na kasi ya maendeleo katika maeneo hayo.

## K. MALENGO YATAYOTEKELEZWA NA IDARA MAALUM ZA SMZ (D02-D06)

78. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Jeshi la Kujenga Uchumi (D02), Chuo cha Mafunzo (D03), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (D04), Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (D05) na Kikosi cha Valantia Zanzibar (D06) malengo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025;-

a) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ziendazo katika Kambi zote za Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

b) Kuimarisha mazingira ya kazi na makaazi ya Maafisa na Wapiganaji kwa kuendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Afisi, nyumba na Mahanga kwa kila Idara Maalum za SMZ ambapo mkazo mkubwa ni kujenga majengo makubwa ya kisasa kulingana na mandhari na haiba ya maeneo husika.

c) Kuimarisha huduma za zimamoto nchini kwa kununua gari za zimamoto na vifaa mbali mbali vya kukabiliana na majanga ya moto sambamba na kuboresha huduma za zimamoto kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amaan Karume kwa kuzingatia hadhi na maendeleo ya uwanja huo.

d) Kusimamia upatikanaji wa gari 17 mpya za kisasa kwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, boti ya zimamoto na vifaa vingine vya uzimaji moto ikiwa ni sehemu ya gawio la mkopo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

e) Kuboresha ulinzi wa mipaka ya bahari ya Zanzibar, kuboresha hifadhi ya rasilimali za bahari pamoja na kudhibiti usafirishaji wa magendo kwa kuhakikisha vyombo vyote vya KMKM vinafanyiwa matengenezo makubwa na kupatiwa mafuta ya kutosha.

f) Kuimarisha mfumo wa Haki Jinai Chuo cha Mafunzo kwa kuifanyia kazi ripoti ya Kitaifa kufuatia Kamati

Maalum iliyoundwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, huduma za urekebishaji tabia za wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo zitaboreshwa ili kuwafanya wanafunzi wanaomaliza kutumikia muda wao kuwa na tabia njema.

g) Kufanya mageuzi ya utoaji wa mafunzo ya ujenzi wa Taifa yanayoendeshwa na Jeshi la Kujenga Uchumi na kuongeza idadi ya vijana kwa kuhakikisha vijana wanaomaliza mafunzo hayo wanajitegemea ipasavvyo. Vilevile, huduma za ulinzi zitolewazo na Wakala wa Ulinzi JKU zitaboreshwa ili kuweza kuhimili ushindani katika soko la wawekezaji na maeneo mengine ya kibiashara kama vile ulinzi kwenye maeneo ya mabenki.

h) Kuimarisha operesheni za kiulinzi zinazoendeshwa na Kikosi cha Valantia Zanzibar pamoja na kukiwezesha Kikosi kufanya operesheni mbalimbali za kuvunja makundi ya uhalifu kwenye maeneo yote ya Zanzibar. Hili litaenda sambamba na kukipatia Kikosi cha KVZ vitendea kazi vya kisasa kutekeleza jukumu hilo.

i) Kuboresha huduma za afya zinazotolewa na vituo vya afya vya Idara Maalum kwa lengo la kupatiwa madaraja na vifaa vya kisasa ili kutoa huduma za viwango vya juu kwa Maafisa, Askari na Wananchi.

j) Kulea na kukuza vipaji vya wanamichezo kwa lengo la kushiriki katika michezo ya mashindano ya Kimataifa na kujenga afya za Maafisa na Wapiganaji wetu.

k) Kuzijengea uwezo kampuni za ujenzi zilizoanzishwa kwenye kila Kikosi ili kuweza kushindana na kutoa huduma za ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

l) Kuandaa miradi ya maendeleo yenye kujiendesha (bankable projects) kwa lengo la kuziwezesha Idara Maalum kupata mapato na kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali kuu.

m) Kukamilisha marekebisho ya Sheria za Idara Maalum za SMZ ili kuziimarisha zaidi katika kutekeleza majukumu mbali mbali.

n) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ ili iweze kuwa na uwezo zaidi wa kisheria kusimamia maslahi na utendaji kazi wa Idara Maalum za SMZ zikiwa ni sehemu ya vyombo vya ulinzi na usalama.

o) Kuendelea na zoezi la upimaji wa maeneo ya Kambi za Idara Maalum za SMZ na kuanzisha Kambi mpya za Idara Maalum za SMZ.

p) Kukamilisha miradi yote ya maendeleo hususan ya Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Idara Maalum za SMZ ambayo ilikuwa haijakamilika.

q) Kuyaboresha maslahi ya Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ katika maeneo yote yanayogusa utendaji wao wa kazi.

## L. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2024/2025

79. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Afisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya malengo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa;-

a) Kuanza taratibu za ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya Unguja na Pemba. Zoezi ambalo litasimamiwa kwa pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

b) Kuimarisha shughuli za kudumisha amani, utulivu, umoja na mshikamano.

c) Kuendelea kushirikiana na sekta mbali mbali za Serikali na binafsi kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli zenye tija kwa jamii.

d) Kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Mikoa.

e) Kufanya suluhu ya migogoro inayojitokeza kwenye maeneo yao ikiwemo migogoro ya ardhi.

f) Kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kufuatia ziara wanazozifanya kwenye Mikoa na Wilaya.

g) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

h) Kusimamia utekelezaji wa mikakati ya Mpango Mkuu wa Kupambana na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto Wilayani.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa malengo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa na Baraza la Jiji, Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri;

a. Kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kukuza mapato na kuzuia upotevu wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa bila ya kuathiri ustawi wa wananchi.

b. Kusimamia kikamilifu mikakati ya kuimarisha usafi wa mazingira katika miji yetu ikiwemo kuzipatia Mamlaka za Serikali za mitaa vifaa vya usafi kwa njia ya mkopo pamoja na kubinafsisha (outsourcing) shughuli za usafi wa mazingira.

c. Kusimamia na kuitunza miundombinu ya masoko, maeneno ya wajasiriamali, bustani na shughuli nyengine za uhifadhi wa afya na mazingira.

d. Kuendeleza zoezi la kuwasajili na kuwaimarisha Wajasiriamali wadogo waliopo Unguja na Pemba.

e. Baraza la Manispaa Mjini litaendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Soko la Mbogamboga la Mombasa kwa kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF); Kujenga Soko la Kwa Haji Tumbo pamoja na kushirikiana

na Muwekezaji AFRICAB kukamilisha ujenzi wa maduka Darajani awamu ya pili.

f. Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limepanga kukamilisha miradi ya Ujenzi wa Stendi ya Daladala Mndo, Ujenzi wa Soko la Mtoni kwa Kisasi na kuanza taratibu za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano Kidichi.

g. Baraza la Manispaa Magharibi 'B' limepanga kuanza ujenzi wa soko dogo na milango ya biashara katika eneo la Kwa Mchina Mwanzo pamoja na ujenzi wa maegesho eneo la Mombasa Sokoni.

h. Baraza la Mji Kati limepanga kuanza ujenzi wa Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Hanyegwa Mchana na kujenga bustani ya umma ya kisasa katika eneo la Tunguu.

i. Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imepanga kukamilisha Ujenzi wa Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Paje pamoja na kuendelea na Ujenzi wa Soko la Kizimkazi awamu ya pili na kukamilisha ujenzi wa vituo 10 vya kusubiria Daladala.

j. Manispaa ya Kaskazini 'A' imepanga kukamilisha ujenzi wa Soko la Mkwajuni na Soko la Chaani na kuanza matayarisho ya ujenzi wa Soko la Nungwi na Soko la Mbuyutende Muyuni.

k. Baraza la Mji Kaskazini B limepanga kuanza ujenzi wa Soko la Bumbwini, ujenzi wa Soko la Mahonda na kukamilisha ujenzi wa Soko la Kitope pamoja na utekelezaji wa miradi midogo ya Wadi.

l. Baraza la Manispaa Chake Chake limepanga kukamilisha Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi, kuanza ujenzi wa Soko la Vitongoji, ujenzi wa Soko la Ndagoni pamoja na kukamilisha Ujenzi wa Maegesho ya Gari Tibirinzi.

m. Baraza la Mji Mkoani limepanga kujenga Soko la Samaki na mbogamboga Kengeja, kutekeleza miradi midogo tisa ya Wadi pamoja na kufanya marejesho ya malipo ya Soko la Mtambile.

n. Baraza la Mji Wete limepanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa Soko la Mzambarauni na Soko la Kojani Kisiwani.

0. Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imepanga kuanza maandalizi ya mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha kufurahishia Watoto Tumbe na kukamilisha ujenzi wa vituo vitano (5) vya kusubiria daladala.

## M. MALENGO YATAKAYOTEKELEZWA NA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII KWA MWAKA 2024/2025

i. Kuweka namba maalum (B1) katika nyaraka ngumu.

ii. Kuendelea kuingiza kumbukumbu za nyaraka ngumu katika Mfumo wa Usajili wa Kielektroniki (Digitization).

iii. Kutunga Kanuni za Ulinzi wa taarifa za Usajili wa matukio ya kijamii.

iv. Kuunganisha mfumo wa usajili wa Matukio ya Kijamii na mifumo ya taasisi nyengine kwa ajili ya kuchangia taarifa (data sharing).

v. Kuanza kuutumia mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kufanya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa kupitia mtandao (online verification).

vi. Kufunga mifumo ya kisasa ya kiusalama katika Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

## N. MAOMBI YA KUIDHINISHIWA MAPATO NA MATUMIZI KWA KILA FUNGU (DO1-D12) KWA MWAKA FEDHA 2024/2025

81. **Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kutekeleza malengo niliyoyataja naliomba Baraza lako kuidhinisha mapato na matumizi ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kila fungu la bajeti kuanzia D01 hadi D12 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama ifuatavyo;-

82. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D01 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Mkuu wa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum

za SMZ linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 97,269,016,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,280,000,000 ni mishahara, Shilingi 4,717,300,000 ni matumizi mengineyo (O.C), Shilingi 151,400,000 ni ruzuku ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ na Shilingi 90,120,316,000 ni kazi za maendeleo ambapo kati ya hizo Shilingi 11,120,316,000 ni fedha za Wahisani.

83. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D02 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamanda Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 45,446,600,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 34,099,200,000 ni mishahara, Shilingi 7,680,000,000 ni matumizi mengineyo, Shilingi 527,400,000 ni ruzuku ya Wakala wa Ulinzi JKU na Shilingi 3,140,000,000 ni kazi za maendeleo. Aidha,fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 2,242,633,000 yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo Shilingi 2,100,000,000 zitakusanywa na Wakala wa Ulinzi na Shilingi 142,633,000 zitachangiwa na Jeshi la Kujenga Uchumi.

84. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D03 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamishna wa Chuo Cha Mafunzo linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 29,880,030,000. Kati ya hizo Shilingi 22,563,800,000 ni mishahara, Shilingi 4,766,230,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 2,550,000,000 ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 173,600,000 yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

85. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D04 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 44,584,040,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 34,990,900,000 ni mishahara, Shilingi 4,483,100,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 5,110,040,000 ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa

mapato ya Shilingi 94,230,000 yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

86. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D05 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 58,207,259,000. Kati ya fedha hizo Shillingi 17,222,600,000 ni mishahara, Shillingi 3,616,000,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 37,368,659,000 ni kazi za maendeleo ambapo kati ya hizo Shilingi 27,140,000,000 ni fedha za Wahisani. Vile vile, Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 153,747,000 yatayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

87. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D06 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi Cha Valantia linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 34,384,300,000. Kati ya fedha hizo Shillingi 22,546,600,000 ni mishahara, Shillingi 3,120,300,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 8,717,400,000 ni kazi za maendeleo.

88. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D07 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mjini Magharibi linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 13,161,800,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,617,700,000 ni mishahara, Shilingi 1,527,800,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 9,016,300,000 ni ruzuku ya Serikali zake za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 1,146,300,000 zitatumika kwa Baraza la Jiji, Shilingi 4,810,400,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa ya Mjini, Shilingi 1,437,800,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Magharibi "A" na Shilingi 1,621,800,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Magharibi "B".

89. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D07 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 54,600,000 yatakayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Fungu D07 linaomba kuidhinishiwa mapato ya ndani Shilingi 4,444,231,455

yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa ya Mjini, mapato ya ndani ya Shilingi 2,316,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Magharibi 'A' na mapato ya ndani ya Shilingi 2,632,591,945 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa ya Magharibi 'B'.

90. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D08 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 4,294,600,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,042,500,000 ni mishahara, Shilingi 557,900,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 1,694,200,000 ni ruzuku ya Serikali zake Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 901,900,000 zitatumika kwa Baraza la Mji Kati na Shilingi 792,300,000 Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.

91. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D08 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 57,035,000 yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Fungu D08 linaomba kuidhinishiwa mapato ya ndani ya Shilingi 1,700,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Kati na mapato ya ndani ya Shilingi 1,023,712,800 yatakayokusanywa na kutumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.

92. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D09 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Unguja linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 5,266,600,000**.** Kati ya fedha hizo Shilingi 2,032,900,000 ni mishahara, Shilingi 767,600,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 2,466,100,000 ni ruzuku ya Serikali zake za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 1,139,200,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Kaskazini "A" na Shilingi 1,088,900,000 zitatumika kwa Baraza la Mji Kaskazini 'B'.

93. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D09 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 37,553,000 yatakayokusanywa kuchangia

Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, fungu D09 pia linaomba kuidhinishiwa mapato ya ndani Shilingi 2,656,001,950 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Kaskazini ‘A’ na mapato ya ndani ya Shilingi 1,824,100,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji kaskazini ‘B’.

94. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D10 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Pemba linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 5,859,000,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,528,700,000 ni mishahara, Shilingi 877,400,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 3,452,900,000 ni ruzuku ya Serikali zake za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 1,959,500,000 zitatumika kwa Baraza la Manispaa Chake Chake na Shilingi 1,284,000,000 zitatumika kwa Baraza la Mji Mkoani.

95. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D10 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 47,116,000 yatakayokusanywa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kadhalika Fungu hili linaomba kuidhinishiwa makusanyo ya ndani ya Shilingi 880,788,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Manispaa Chake Chake na Shilingi 547,075,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Mkoani.

96. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D11 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Pemba linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 5,012,700,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,493,200,000 ni mishahara, Shilingi 943,200,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 2,576,300,000 ni ruzuku ya Serikali zake za Mitaa. Kati ya fedha hizo za ruzuku Shilingi 1,564,100,000 zitatumika kwa Baraza la Mji Wete na Shilingi 1,012,200,000 zitatumika kwa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

97. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D11 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 17,358,000 yatakayokusanywa kuchangia

katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Vilevile Fungu hili linaomba kuidhinishiwa mapato ya ndani ya Shilingi 500,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Baraza la Mji Wete na mapato ya ndani ya Shilingi 420,000,000 yatakayokusanywa na kutumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

98. **Mheshimiwa Spika,** Fungu D12 ambalo mapato na matumizi yake yatasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar linaomba kuidhinishiwa matumizi ya Shilingi 6,646,800,000. Kati ya fedha hizo Shilingi 2,873,100,000 ni mishahara, Shilingi 1,873,700,000 ni matumizi mengineyo na Shilingi 1,900,000,000 ni kazi za maendeleo. Aidha, Fungu D12 linaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 2,231,810,000 yatakayokusanywa kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali. **(Kiambatanisho nambari 10,11,12 na 13)**

## O. SHUKRANI

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa kipekee natoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi wa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango chini ya usimamizi makini wa Mheshimiwa Waziri Dkt Saada Mkuya Salum na Katibu Mkuu wake Dkt Juma Malik Akili. Aidha, naishukuru Tume ya Mipango Zanzibar inayoongozwa na Mwenyekiti wake Dkt Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mtendaji wa Tume Dkt Rahma Salim Mahfoudh. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Dkt Mwinyi Talib Haji Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushauri wa kisheria katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

100. **Mheshimiwa Spika,** nimelazimika kutoa shukurani kwa Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa sababu ya mashirikiano makubwa tuliyopeana kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ushauri wao, uthubutu na uzalendo wao umetuwezesha kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli nyengine mahsusi kwa ufanisi na uweledi. Nategemea mashirikiano

hayo yataongezeka maradufu katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa namna alivyofuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo hasa ujenzi wa masoko ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.

101. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutumia fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa misaada na michango yao katika kuchangia maendeleo ya kitaifa kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Miongoni mwa Washirika hao ni pamoja na; Ubalozi wa China, Umoja wa Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Kimataifa la (UNFPA), Shirika la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Serikali ya Austria, Taasisi za Kifedha, Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs) pamoja na Washirika wote ambao sikuweza kuwataja hapa.

102. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru watendaji wa Ofisi hii na Taasisi zilizo chini yake kwa kufanya kazi kwa umahiri, weledi, ufanisi na moyo wa uzalendo kwa maslahi ya Taifa letu. Shukrani maalum nazitoa kwa Katibu Mkuu Ndugu Issa Mahfoudh Haji, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mikidadi Mbarouk Mzee, Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Idara za Makao Makuu, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mameya na Wenyeviti wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Masheha.

103. **Mheshimiwa Spika,** niendelee pia kutoa shukurani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na Naibu Mkurugenzi wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Viwanda vya Idara Maalum za SMZ, Mkurugenzi wa Wakala wa Ulinzi JKU, Mwenyeviti wa Bodi wa Wakala wa Ulinzi JKU, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii pamoja na watendaji wote.

104. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukurani zangu kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Ole kwa imani yao na mashirikiano wanayoendelea kunipatia wakati nikiendelea kutekeleza majukumu niliyopatiwa na waliyonipatia kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Vile vile, naishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao wanaonionyesha wakati nikiendelea kutekeleza majukumu ya Kitaifa. Aidha, navishukuru vyombo vya habari kwa mchango wao katika kuhabarisha Wananchi juu ya matukio mbali mbali yanayohusu Wizara hii.

## P. HITIMISHO

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya Shilingi **350,012,745,000.** Kati ya fedha hizo Shilingi 146,291,200,000 kwa ajili ya mishahara, Shilingi 34,930,530,000 kwa matumizi mengineyo, Shilingi 19,884,600,000 ruzuku kwa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ, Wakala wa Ulinzi wa JKU na Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Shilingi 148,906,415,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Aidha, Afisi inaomba kuidhinishiwa mapato ya Shilingi 5,109,682,000 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali, na mapato ya ndani ya Shilingi 18,944,501,150 yatakayokusanywa na kutumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

106. **Mheshimiwa Spika** na Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

**MASOUD ALI MOHAMMED**
**WAZIRI WA NCHI**
**AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA**
**NA IDARA MAALUM ZA SMZ**
**ZANZIBAR**

**Kiambatisho namba 1: MAPATO YALIYOKUSANYWA NA KUPELEKWA HAZINA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI MACHI 2023/2024**

| | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MIEZI 9 JULAI-MACHI 2023/2024 | MAKUSANYO KWA MWAKA 2023/2024 | ASILIMIA YA MAKUSANYO MIEZI 9 2023/2024 | ASILIMIA YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 135,000,000 | 101,250,000 | 95,360,000 | 94 | 71 |
| | Wakala wa ulinzi JKU | 1,923,234,000 | 1,442,425,500 | 506,697,495 | 35 | 26 |
| D03 | Chuo Cha Mafunzo | 131,903,878 | 98,927,909 | 95,320,500 | 96 | 72 |
| D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 87,982,000 | 65,986,500 | 36,659,167 | 56 | 42 |
| D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 113,194,000 | 84,895,500 | 93,191,000 | 110 | 82 |
| D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 75,801,000 | 56,850,750 | 20,838,400 | 37 | 27 |
| D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 45,248,000 | 33,936,000 | 15,426,000 | 45 | 34 |
| D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 37,859,000 | 28,394,250 | 4,820,000 | 17 | 13 |
| D10 | Mkoa Wa Kusini Pemba | 57,846,000 | 43,384,500 | 8,246,257 | 19 | 14 |
| D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 25,000,000 | 18,750,000 | 9,000,000 | 48 | 36 |
| D12 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 1,570,000,000 | 1,177,500,000 | 1,039,861,608 | 88 | 66 |
| | **JUMLA KUU** | **4,203,067,878** | **3,152,300,909** | **1,925,420,427** | 61 | 46 |

**Kiambatisho namba 2: MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MATUMIZI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2023/2024**

| NA | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MIEZI TISA(9) | MAKUSANYO JULAI HADI MACHI 2023/2024 | ASILIMIA YA MAKUSANYO KWA MIEZI 9 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BARAZA LA MANISPAA MJINI | 5,252,940,000 | 3,785,935,000 | 2,090,448,306 | 55 |
| 2 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | 2,000,000,000 | 1,500,000,000 | 1,087,190,883 | 72 |
| 3 | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,928,000,000 | 2,209,060,000 | 1,682,338,706 | 76 |
| 4 | BARAZA LA MJI KATI | 1,672,000,000 | 1,150,278,650 | 1,029,075,978 | 89 |
| 5 | HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI | 957,920,000 | 514,011,774 | 429,790,087 | 84 |
| 6 | BARAZA LA MJI KASKAZINI A | 1,340,063,900 | 1,050,736,925 | 978,595,347 | 93 |
| 7 | BARAZA LA MJI KASKAZINI B | 1,674,000,000 | 1,255,500,000 | 883,368,948 | 70 |
| 8 | BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE | 859,428,000 | 664,777,877 | 631,977,055 | 95 |
| 9 | BARAZA LA MJI MKOANI | 537,086,000 | 402,814,500 | 317,596,650 | 79 |
| 10 | BARAZA LA MJI WETE | 474,000,000 | 363,592,000 | 333,145,128 | 92 |
| 11 | HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI | 420,000,000 | 320,000,000 | 224,735,865 | 70 |
|  | **JUMLA** | **18,115,437,900** | **13,216,706,726** | **9,688,262,952** | **73** |

## Kiambatisho namba 3a : MCHANGANUO WA MATUMIZI YA FEDHA KWA TAASISI ZA OR-TMSMIM KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| | TAASISI | MAKADIRIO YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024 | | | | | MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024 | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MSHAHARA | OC | RUZUKU | MAENDELEO | JUMLA | MSHAHARA | % | OC | % | RUZUKU | % | MAENDELEO | % | JUMLA | % |
| D01 | Idara za Ofisi Kuu | 2,169,900,000 | 3,628,700,000 | 137,600,000 | 28,000,000,000 | 33,936,200,000 | 1,596,848,628 | 74 | 919,197,000 | 25 | 65,652,400 | 48 | 61,348,516,014 | 219 | 63,930,214,042 | 188 |
| **Jumla Ndogo Afisi Kuu** | | **2,169,900,000** | **3,628,700,000** | **137,600,000** | **28,000,000,000** | **33,936,200,000** | **1,596,848,628** | **74** | **919,197,000** | **25** | **65,652,400** | **48** | **61,348,516,014** | **219** | **63,930,214,042** | **188** |
| D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) | 29,798,100,000 | 6,400,000,000 | 479,400,000 | 3,000,000,000 | 39,677,500,000 | 23,503,069,866 | 79 | 4,410,837,240 | 69 | 157,885,000 | 33 | 0 | 0 | 28,071,792,106 | 71 |
| D03 | Chuo Cha Mafunzo | 19,960,400,000 | 3,934,300,000 | 0 | 1,500,000,000 | 25,394,700,000 | 15,477,597,462 | 78 | 2,344,000,000 | 60 | 0 | O | 1,457,042,825 | 97 | 19,278,640,287 | 76 |
| D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 31,384,400,000 | 3,735,900,000 | 0 | 2,500,000,000 | 37,620,300,000 | 24,182,696,710 | 77 | 2,501,124,619 | 67 | 0 | 0 | 2,325,000,000 | 93 | 29,008,821,329 | 77 |
| D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 14,312,600,000 | 2,012,400,000 | 0 | 3,500,000,000 | 19,825,000,000 | 11,733,684,176 | 82 | 1,512,139,217 | 75 | 0 | 0 | 622,029,000 | 18 | 13,867,852,393 | 70 |
| D06 | Kikosi cha Valantia | 19,524,800,000 | 2,228,800,000 | 0 | 1,500,000,000 | 23,253,600,000 | 15,443,567,749 | 79 | 1,931,000,000 | 87 | 0 | 0 | 396,108,300 | 26 | 17,770,676,049 | 76 |
| **Jumla Idara Maalum** | | **114,980,300,000** | **18,311,400,000** | **479,400,000** | **12,000,000,000** | **145,771,100,000** | **90,340,615,963** | **79** | **12,699,101,076** | **69** | **157,885,000** | **33** | **4,800,180,125** | **40** | **107,997,782,164** | **74** |
| D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 2,358,000,000 | 1,062,300,000 | 8,530,800,000 | 0 | 11,951,100,000 | 1,813,123,978 | 77 | 376,470,000 | 35 | 6,008,816,993 | 70 | 0 | 0 | 8,198,410,971 | 69 |
| D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 2,902,500,000 | 286,400,000 | 1,936,900,000 | 0 | 5,125,800,000 | 1,382,006,838 | 48 | 147,000,000 | 51 | 1,102,980,769 | 57 | 0 | 0 | 2,631,987,607 | 51 |
| D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 1,956,400,000 | 525,100,000 | 2,269,800,000 | 0 | 4,751,300,000 | 1,346,153,565 | 69 | 213,000,000 | 41 | 1,676,437,423 | 74 | 0 | 0 | 3,235,590,988 | 68 |
| D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 1,428,200,000 | 622,600,000 | 3,127,800,000 | 0 | 5,178,600,000 | 1,055,747,019 | 74 | 250,000,000 | 40 | 2,151,225,001 | 69 | 0 | 0 | 3,456,972,020 | 67 |
| D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 1,462,800,000 | 581,700,000 | 2,338,200,000 | 0 | 4,382,700,000 | 1,056,725,177 | 72 | 273,855,000 | 47 | 1,607,141,426 | 69 | 0 | 0 | 2,937,721,603 | 67 |
| **Jumla Mikoa** | | **10,107,900,000** | **3,078,100,000** | **18,203,500,000** | **0** | **31,389,500,000** | **6,653,756,577** | **66** | **1,260,325,000** | **41** | **12,546,601,612** | **69** | **0** | **0** | **20,460,683,189** | 65 |
| D12 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 2,635,300,000 | 1,561,500,000 | 0 | 950,000,000 | 5,146,800,000 | 2,045,902,815 | 78 | 592,235,478 | 38 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2,638,138,293 | 51 |
| | **Jumla Kuu** | **129,893,400,000** | **26,579,700,000** | **18,820,500,000** | **40,950,000,000** | **216,243,600,000** | **100,637,123,983** | **77** | **15,470,858,554** | **58** | **12,770,139,012** | **68** | **66,148,696,139** | **162** | **195,026,817,688** | 90 |

**Kiambatisho Namba 3b : UPATIKANAJI WA MAPATO NA RUZUKU KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

| MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI 2023/2024 | | | | | MAPATO NA MATUMIZI HALISI 2023/2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | TAASISI | RUZUKU | MAPATO YA NDANI | JUMLA | RUZUKU | % | MAPATO YA NDANI | % | JUMLA | % |
| 1. | BARAZA LA MANISPAA MJINI | 4,451,800,000 | 5,252,940,000 | 9,704,740,000 | 3,233,454,432 | 73 | 2,090,448,306 | 40 | **5,323,902,738** | 55 |
| 2. | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | 1,320,200,000 | 2,000,000,000 | 3,320,200,000 | 986,800,557 | 75 | 1,087,190,883 | 54 | **2,073,991,440** | 62 |
| 3. | BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 1,676,000,000 | 2,928,000,000 | 4,604,000,000 | 1,105,732,216 | 66 | 1,682,338,706 | 57 | **2,788,070,922** | 61 |
| 4. | BARAZA LA MJI KATI | 962,516,000 | 1,672,000,000 | 2,634,516,000 | 620,771,898 | 64 | 1,029,075,978 | 62 | **1,649,847,876** | 63 |
| 5. | HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI | 974,384,000 | 957,920,000 | 1,932,304,000 | 446,154,222 | 46 | 429,790,087 | 45 | **875,944,309** | 45 |
| 6. | BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI A | 1,108,200,000 | 1,340,063,900 | 2,448,263,900 | 828,095,802 | 75 | 978,595,347 | 73 | **1,806,691,149** | 74 |
| 7. | BARAZA LA MJI KASKAZINI B | 1,161,600,000 | 1,674,000,000 | 2,835,600,000 | 848,341,621 | 73 | 883,368,948 | 53 | **1,731,710,569** | 61 |
| 8. | BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE | 1,875,700,000 | 859,428,000 | 2,735,128,000 | 1,119,141,944 | 60 | 631,977,055 | 74 | **1,751,118,999** | 64 |
| 9. | BARAZA LA MJI MKOANI | 1,150,278,650 | 537,086,000 | 1,687,364,650 | 934,558,057 | 81 | 317,596,650 | 59 | **1,252,154,707** | 74 |
| 10. | BARAZA LA MJI WETE | 1,367,800,000 | 474,000,000 | 1,841,800,000 | 996,613,391 | 73 | 333,145,128 | 70 | **1,329,758,519** | 72 |
| 11. | HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI | 809,900,000 | 420,000,000 | 1,229,900,000 | 488,153,035 | 60 | 224,735,865 | 54 | **712,888,900** | 58 |
| **JUMLA** | | **16,858,378,650** | **18,115,437,900** | **34,973,816,550** | **11,607,817,175** | **69** | **9,688,262,952** | **53** | **21,296,080,127** | **61** |

**Kiambatanisho namba 4: IDADI YA SHEHIA ZINAZOJENGWA KWA MWAKA 2023/2024 NA SHEHIA ZITAKAZOJENGWA KWA MWAKA 2024/2025**

**IDADI YA OFISI ZA SHEHIA ZINAZOENDELEA KUJENGWA**

| NAM. | SHEHIA | WILAYA |
|---|---|---|
| 1. | Shehia ya Jitimai | Wilaya ya Magharibi "B" |
| 2. | Shehia ya Fumba | Wilaya ya Magharibi "B" |
| 3. | Shehia ya Shakani | Wilaya ya Magharibi "B" |
| 4. | Shehia ya Jang'mbe | Wilaya ya Mjini |
| 5. | Shehia ya Miembeni | Wilaya ya Mjini |
| 6. | Shehia ya Kijini | Wilaya ya Kaskazini "A" |

**IDADI YA OFISI ZA SHEHIA ZITAKAZOJENGWA KWA MWAKA 2023/2024**

| SHEHIA ZA UNGUJA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | SHEHIA | WILAYA | | SHEHIA | WILAYA |
| 1 | Mikunguni | Mjini | 18. | Fujoni | Kaskazini "B" |
| 2 | Maruhubi | | 19. | Kidazini | |
| 3 | Kwaalinatu | | 20. | Matetema | |
| 4 | | | 21. | Kinduni | |
| 5 | Kianga | Magharibi "A" | 22. | Kiombamvua | |
| 6 | Munduli | | 23. | Mkadini | |
| 7 | Dole | | 24. | Kizimkazi Mkunguni | Kusini |
| 8 | Kizimbani | | 25. | Muyuni B | |
| 9. | Mfeneseni | | 26. | Muyuni C | |
| 10 | Mambosasa | Magharibi "B" | 27 | Mzuri | |
| 11 | Kwamchina | | 28. | Paje | |
| 12 | Mombasa | | 29. | Uzi Ng'ambwa | Kati |
| 13 | Kidombo | Kaskazini "A" | 30. | UKongoroni | |
| 14 | Tazari | | 31. | Ndijani Mseweni | |
| 15 | Chaani Masingini | | 32 | Chwaka | |
| 16 | Kivunge | | 33. | Jendele | |
| 17 | Tumbatu Jongowe | | 34 | Pagali | |

| SHEHIA ZA PEMBA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | SHEHIA | WILAYA | | SHEHIA | WILAYA |
| 1 | Ndagoni | Chake Chake | 13 | Piki | Wete |
| 2 | Gombani | | 14. | Kinyasini | |
| 3 | Ziwani | | 15. | Junguni | |
| 4 | Ole | | 16. | Kipangani | |
| 5 | Mjini OLe | | 17. | Shengejuu | |
| 6 | Pujini | | 18. | Pandani | |
| 7 | Michezani | Mkoani | 19. | Konde | Michweni |
| 8 | Chambani | | 20. | Kipange | |
| 9. | Kendwa | | 21. | Msuka Magharibi | |
| 10. | Mjimbini | | 22. | Kinyasini | |
| 11. | Kengeja | | 23. | Maziwa Ng'ombe | |
| 12. | Dodo | | 24. | Wingwi Mtemani | |

**SHEHIA ZINAZOTARAJIWA KUJENGWA KWA MWAKA 2024/2025**

| **SHEHIA ZA UNGUJA** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Nam.** | **SHEHIA** | **WILAYA** | **Nam.** | **SHEHIA** | **WILAYA** |
| | BUMBWISUDI | MAGHARIBI A | | TUNGUU | KATI |
| | MWAKAJE | | | BUNGI | |
| | MWERA | | | JUMBI | |
| | MTOFAANI | | | KOANI | |
| | KISAUNI | MAGHARIBI B | | MAKUNDUCHI | KUSINI |
| | KIPUNGANI | | | DONGWE | |
| | KIBONDENI | | | KITOGANI | |
| | MNARANI | | | KIBUTENI | |
| | MOMBASA | | | | |
| | MATEMWE KASKAZINI | KASKAZINI "A" | | DONGE NJIA YA MTONI | KASKAZINI "B" |
| | MATEMWE MBUYU TENDE | | | KIONGWE KIDOGO | |
| | POTOA | | | KITOPE | |
| | MOGA | | | MAHONDA | |
| | BANDAMAJI | | | MANGAPWANI | |
| **JUMLA** | | | | | **28** |

| **SHEHIA ZA PEMBA** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Nam.** | **SHEHIA** | **WILAYA** | **Nam.** | **SHEHIA** | **WILAYA** |
| | MGELEMA | CHAKE CHAKE | | FUNDO | WETE |
| | MATALE | | | KAMBINI | |
| | MFIKIWA | | | MCHANGA MDOGO | |
| | MCHANGAMRIMA | | | PEMBENI | |
| | KWALE | | | KOJANI | |
| | MINAZINI | MKOANI | | CHIMBA | MICHEWENI |
| | CHUMBAGENI | | | SHUMBA VYAMBONI | |
| | MWAMBE | | | KINOE | |
| | KIWANI | | | TUMBE MASHARIKI | |
| | MIZINGANI | | | KIUYU MBUYUNI | |
| | **JUMLA** | | | | **20** |
| | **JUMLA UNGUJA NA PEMBA** | | | | **48** |

**Kiambatanisho namba 5: IDADI YA MAAFISA NA WAPIGANAJI WA IDARA MAALUM ZA SMZ WALIOPANDISHWA VYEO**

| NAM | IDARA | MAAFISA WALIOPANDISHWA VYEO NA KAMANDA MKUU WA IDARA MAALUM | | | MAAFISA WALIOPANDISHWA VYEO NA TUME YA UTUMISHI YA IDARA MAALUM | | | WAPIGANAJI WALIOPANDISHWA VYEO NA WAKUU WA IDARA MAALUM | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA | |
| 1 | KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO | 11 | 3 | 14 | 32 | 20 | 52 | 660 | 125 | 785 | 851 |
| 2 | JESHI LA KUJENGA UCHUMI | 6 | 8 | 14 | 26 | 17 | 43 | 394 | 117 | 511 | 568 |
| 3 | CHUO CHA MAFUNZO | 4 | 2 | 6 | 17 | 9 | 26 | 331 | 76 | 407 | 439 |
| 4 | KIKOSI CHA ZIMAMMOTO NA UOKOZI | 12 | 5 | 17 | 12 | 7 | 19 | 141 | 80 | 221 | 257 |
| 5 | KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR | 6 | 3 | 9 | 4 | 4 | 8 | 449 | 71 | 520 | 537 |
| **JUMLA** | | **39** | **21** | **60** | **91** | **57** | **148** | **1,975** | **469** | **2,444** | **2,652** |

**Kiambatanisho namba 6: JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI ZILIZOTOA MCHANGO WA MAENDELEO 2023/2024**

| MAJINA YA JUMUIYA | | AINA YA MIRADI ILIYOTEKELEZWA | FEDHA ZILIZOTUMIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | COMMUNITY FORESTS PEMBA | MAZINGIRA | 4,163,879,468.72 |
| 2. | NOOR AL YAKINI | DINI | 3,546,790,000 |
| 3. | ASSALAM COMMUNITY FOUNDATION | HUDUMA ZA JAMII | 2,762,131,460 |
| 4. | OIKOS EAST AFRICA | MAZINGIRA | 2,685,000,000 |
| 5. | TURKISH MAARIF FOUNDATION | ELIMU | 2,598,032,957 |
| 6. | MILELE ZANZIBAR | HUDUMA ZA JAMII | 2,494,798,562 |
| 7. | EPHATA NATIONAL DEVELOPMENT SERVICES | ELIMU | 1,337,916,426 |
| 8. | MUZDALIFA CHARITABLE ORGANIZATION | HUDUMA ZA JAMII | 896,884,900 |
| 9. | ZANZIBAR MAISHA BORA FOUNDATION (ZBMF) | HUDUMA ZA JAMII | 879,215,532 |
| 10. | IMPACT ZANZIBAR | AFYA | 604,120,974 |
| 11. | THE WORLD UNITE FOR ENVIRONMENT AND SOCIAL SUSTANABILITY | MAZINGIRA | 600,000,000 |
| 12. | WAJAMAMA | AFYA | 497,653,181 |
| 13. | ASMA MWINYI FOUNDATION | HUDUMA ZA JAMII | 467,341,400 |
| 14. | ZOP | AFYA | 459,552,667 |
| 15. | MISHKAT FOUNDATION | MAENDELEO YA JAMII | 438,977,650 |
| 16. | JUMUIYA ZILIZOBAKIA | | 34,197,453,676.28 |
| | **JUMLA KUU** | | **58,629,748,854** |

**Kiambatanisho namba 7: IDADI YA MAAFISA NA WAPIGANAJI WALIOJENGEWA UWEZO 2023/2024**

| NAM | IDARA | AINA YA MAFUNZO | | | | | | | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | UONGOZI MKUBWA | | | UONGOZI WA KATI | | | MAFUNZO YA KITAALUMA | | | |
| | | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA | |
| 1. | JESHI LA KUJENGA UCHUMI | 202 | 44 | 246 | 0 | 0 | 0 | 8 | 6 | 14 | **260** |
| 2. | KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO | 0 | 0 | 0 | 53 | 17 | 70 | 59 | 15 | 74 | **144** |
| 3. | CHUO CHA MAFUNZO | 0 | 0 | 0 | 231 | 61 | 292 | 1 | 1 | 2 | **294** |
| 4. | KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI | 0 | 0 | 0 | 108 | 38 | 146 | 36 | 14 | 50 | **196** |
| 5. | KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR | 179 | 32 | 211 | 0 | 0 | 0 | 11 | 5 | 16 | **227** |
| | **JUMLA KUU** | **381** | **76** | **457** | **392** | **116** | **508** | **115** | **41** | **156** | **1121** |

**Kiambatanisho namba 8: TAKWIMU ZA VIKAO VYA KAMATI ZA ULINZI NA USALAMA KATIKA MIKOA**

| MKOA | IDADI YA VIKAO | VIKAO VYA KAWAIDA | VIKAO VYA DHARURA |
|---|---|---|---|
| MJINI MAGHARIBI | 41 | 28 | 13 |
| **KUSINI UNGUJA** | 12 | 9 | 3 |
| **KASKAZINI UNGUJA** | 34 | 27 | 7 |
| **KASKAZINI PEMBA** | 59 | 27 | 32 |
| **KUSINI PEMBA** | 13 | 9 | 4 |
| **JUMLA** | **159** | **100** | **59** |

**Kiambatanisho namba 9: TAKWIMU ZA USULUHISHI WA MIGOGORO YA ARDHI KATIKA MIKOA**

| MKOA | JUMLA YA MIGOGORO ILIYORIPOTIWA | ILYOPATIWA UFUMBUZI | INAYOENDELEA NA HATUA ZA USULUHISHI |
|---|---|---|---|
| **MJINI MAGHARIBI** | 65 | 6 | 59 |
| **KUSINI UNGUJA** | 21 | 0 | 21 |
| **KASKAZINI UNGUJA** | 29 | 13 | 16 |
| **KASKAZINI PEMBA** | 31 | 29 | 2 |
| **KUSINI PEMBA** | 31 | 13 | 18 |
| **JUMLA** | **177** | **61** | **116** |

**Kiambatisho Namba 10: MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA RUZUKU KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| TAASISI | MAKUSANYO 2024/2025 | RUZUKU 2024/2025 |
|---|---:|---:|
| BARAZA LA MANISPAA MJINI | 4,444,231,455 | 4,810,400,000 |
| BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI A | 2,316,000,000 | 1,437,800,000 |
| BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI B | 2,632,591,945 | 1,621,800,000 |
| HALMASHAURI YA WILAYA KUSINI | 1,023,712,800 | 901,900,000 |
| BARAZA LA MJI KATI | 1,700,000,000 | 792,300,000 |
| BARAZA LA MANISPAA KASKAZINI A | 2,656,001,950 | 1,139,200,000 |
| BARAZA LA MJI KASKAZINI B | 1,824,100,000 | 1,088,900,000 |
| BARAZA LA MANISPAA CHAKE CHAKE | 880,788,000 | 2,082,500,000 |
| BARAZA LA MJI MKOANI | 547,075,000 | 1,370,400,000 |
| BARAZA LA MJI WETE | 500,000,000 | 1,564,100,000 |
| HALMASHAURI YA WILAYA MICHEWENI | 420,000,000 | 1,012,200,000 |
| **JUMLA KUU** | **18,944,501,150** | **17,821,500,000** |

**Kiambatisho Namba 11: MAPATO YATAKAYOKUSANYWA NA KUPELEKWA MFUKO MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA 2024/2025**

| NAM | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|
| 1 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 142,633,000 |
| 2 | Wakala wa ulinzi JKU | 2,100,000,000 |
| 3 | Chuo Cha Mafunzo | 173,600,000 |
| 4 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 94,230,000 |
| 5 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 153,747,000 |
| 6 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 54,600,000 |
| 7 | Mkoa wa Kusini Unguja | 57,035,000 |
| 8 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 37,553,000 |
| 9 | Mkoa Wa Kusini Pemba | 47,116,000 |
| 10 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 17,358,000 |
| 11 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 2,231,810,000 |
| **JUMLA KUU** | | **5,109,682,000** |

**Kiambatisho Namba 12: MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| FUNGU | TAASISI | JINA LA MRADI | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| D01 | **Idara za Makao Makuu** | Ujenzi wa Ofisi za Shehia | 3,000,000,000 |
| | | Ujenzi wa kituo cha Daladala na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri | 29,000,000,000 |
| | | Kuimarisha Ulinzi na Usalama | 25,000,000,000 |
| | | Kuimarisha Haki jinai katika Chuo cha Mafunzo | 22,000,000,000 |
| | | Mradi wa Green & Smart Cities-SASA | 11,120,316,000 |
| | **Jumla D01** | | **90,120,316,000** |
| **D02** | **Jeshi la Kujenga Uchumi** | Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU | 3,140,000,000 |
| **D03** | **Chuo Cha Mafunzo** | Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga | 2,550,000,000 |
| **D04** | **Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo** | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 5,110,040,000 |
| **D05** | **Kikosi cha Zimamoto na Uokozi** | Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Askari | 10,228,659,000 |
| | | Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto | 27,140,000,000 |
| **D06** | **Kikosi cha Valantia** | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga | 8,717,400,000 |
| **D12** | **Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii** | Mradi wa kuimarisha mifumo ya Usaliji ya Matukio ya Kijamii | 1,900,000,000 |
| | **JUMLA KUU** | | **148,906,415,000** |

**Kiambatisho Namba 13: MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/2025**

| IDARA | KAZI ZA KAWAIDA | | | | KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MSHAHARA NA STAHIKI | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA MISHAHARA &OC | RUZUKU | SMZ | WAHISANI | JUMLA MAENDELEO | JUMLA KUU |
| Afisi Kuu | 2,280,000,000 | 4,717,300,000 | 6,997,300,000 | 151,400,000 | 79,000,000,000 | 11,120,316,000 | 90,120,316,000 | 97,269,016,000 |
| Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) | 34,099,200,000 | 7,680,000,000 | 41,779,200,000 | 527,400,000 | 3,140,000,000 | 0 | 3,140,000,000 | 45,446,600,000 |
| Chuo Cha Mafunzo | 22,563,800,000 | 4,766,230,000 | 27,330,030,000 | 0 | 2,550,000,000 | 0 | 2,550,000,000 | 29,880,030,000 |
| Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 34,990,900,000 | 4,483,100,000 | 39,474,000,000 | 0 | 5,110,040,000 | 0 | 5,110,040,000 | 44,584,040,000 |
| Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 17,222,600,000 | 3,616,000,000 | 20,838,600,000 | 0 | 10,228,659,000 | 27,140,000,000 | 37,368,659,000 | 58,207,259,000 |
| Kikosi cha Valantia | 22,546,600,000 | 3,120,300,000 | 25,666,900,000 | 0 | 8,717,400,000 | 0 | 8,717,400,000 | 34,384,300,000 |
| **Jumla Idara Maalum** | **131,423,100,000** | **23,665,630,000** | **155,088,730,000** | **527,400,000** | **29,746,099,000** | **27,140,000,000** | **56,886,099,000** | **212,502,229,000** |
| Mkoa wa Mjini Magharibi | 2,617,700,000 | 1,527,800,000 | 4,145,500,000 | 9,016,300,000 | 0 | 0 | 0 | 13,161,800,000 |
| Mkoa wa Kusini Unguja | 2,042,500,000 | 557,900,000 | 2,600,400,000 | 1,694,200,000 | 0 | - | - | 4,294,600,000 |
| Mkoa wa Kaskazini Unguja | 2,032,900,000 | 767,600,000 | 2,800,500,000 | 2,466,100,000 | 0 | 0 | 0 | 5,266,600,000 |
| Mkoa wa Kusini Pemba | 1,528,700,000 | 877,400,000 | 2,406,100,000 | 3,452,900,000 | - | - | - | 5,859,000,000 |
| Mkoa wa Kaskazini Pemba | 1,493,200,000 | 943,200,000 | 2,436,400,000 | 2,576,300,000 | 0 | 0 | 0 | 5,012,700,000 |
| **Jumla Mikoa** | **9,715,000,000** | **4,673,900,000** | **14,388,900,000** | **19,205,800,000** | **0** | **0** | **0** | **33,594,700,000** |
| Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 2,873,100,000 | 1,873,700,000 | 4,746,800,000 | 0 | 1,900,000,000 | 0 | 1,900,000,000 | 6,646,800,000 |
| **Jumla Kuu** | **146,291,200,000** | **34,930,530,000** | **181,221,730,000** | **19,884,600,000** | **110,646,099,000** | **65,400,316,000** | **148,906,415,000** | **350,012,745,000** |